**Kabla yakipindi cha Mafunzo kinachofuata, kamilisha hatua za vitendo zifuatazo**.

- Endelea kuuboresha ushuhuda wako ili uakisi maelekezo vizuri katika “Kuandaa na Kushirikisha Ushuhuda Wako Binafsi.”
- Fanya mazoezi ya kuusema ushuhuda wako kwa sauti ukiwa peke yako mpaka utakapokuwa tayari kuushirikisha kwa mtu mwingine.
- Mwombe Mungu aandae “miadi ya Ki-Ungu” kwa ajili yako ili kushirikisha ushuhuda wako (labda pasipo tahadhari yoyote ya mapema) ndani ya majuma manne yajayo.
- Shirikisha ushuhuda wako kwa watu angalau 5 ambao ni marafiki zako wasio Wakristo au utakaokutana nao ndani ya juma lijalo. Toa ushuhuda wako kwa watu wengine watano zaidi ambao sio Wakristo katika eneo lako lengwa kwa ajili ya Kanisa lako jipya kabla ya kipindi cha somo linalofuata.
- Mchukue muumini pamoja nawe kama mlelewa unapowatembelea watu.
- Jiandae kushirikisha ushuhuda wako tena wakati wa kipindi cha mafunzo kinachofuata au wakati wa semina.

# KIPINDI CHA 3
# KUONGOZA VIKUNDI VIDOGO (DK. 60)

**Dhana za Jumla za Uongozi (Dakika 20)**

1. ______________________ katika Maisha ya Kikristo
   - Jukumu la kuwa kielelezo katika uongozi wa Agano Jipya lilikuwa ni lipi? 1 Thes. 1:6-7; 1 Kor. 11:1

2. ___________ Viongozi Wapya
   - Kiongozi wa wanafunzi wapya kwa ajili ya kikundi kidogo ni yupi?
   - Kiongozi wa kikundi kidogo azingatie sifa zipi anapochagua kiongozi wa wanafunzi wapya?
   - Je, kiongozi wa kikundi kidogo agawe shughuli na wajibu kwa washirika wote wa kikundi kidogo, na sio kwa kiongozi wa wanafunzi wapya( kiongozi anayefunzwa kuongoza kikundi kidogo)? Kwa nini ndiyo au kwa nini siyo?
   - Baada ya kikundi kuanza, kiongozi wa kikundi kidogo asubiri kwa muda gani hadi anapochagua kiongozi wa wanafunzi wapya?
   - Ni aina gani ya shughuli ambazo kiongozi wa kikundi kidogo anaweza kuzifanya pamoja na kiongozi wa wanafunzi wapya ili kumwandaa kuongoza kikundi kipya?

3. __________ na ______________ kwa ajili ya Huduma
   - Vikundi vidogo vinasaidia kuandaa viongozi kwa kutoa fursa kwa ajili ya uongozi ndani ya kikundi. Ni aina gani ya mambo ambayo kiongozi mpya atajifunza kutokana na majukumu yanayotendwa katika kikundi kidogo? Toa mifano.

**Kuongoza mikutano ya Vikundi vidogo (Dakika 5)**

1. ______________ na kushirikishana kati ya wanachama wa kikundi.
2. ___________ inayohusisha maombi, kuimba, na kumsifu Mungu.
3. ______________________ na kujadiliana.
4. ___________________________, mahali ambapo wanachama wanajadili shughuli za binafsi na za vikundi ili kuwafikia marafiki, majirani, na labda makundi makubwa kwa injili. Hii inaweza kuhusisha pia muda wa maombi kwa ajili watu fulani maalumu ambao bado hawajaalikwa kwenye kikundi.

**Utawala wa Kikundi Kidogo**

- Kwa nini kiongozi wa kikundi kidogo ajisumbue kuanzisha mpango kwa ajili ya kundi kwa ujumla na kwa ajili ya kila mkutano? Kwa nini asiliache kundi liendelee “kama kawaida” katika mwelekeo liutakao?
- Ni aina gani ya maandalizi yanatakiwa ili kwamba kila mkutano wa kikundi kidogo ukutane na mahitaji yafuatayo?

A. Eneo
B. Ushirika
C. Ibada
D. Maombi
E. Mjadala wa Biblia
F. Mafundisho
G. Uinjilisti

- Kwa nini ni muhimu kila mshirika mpya wa kikundi aandaliwe "mzazi" wa kiroho atakayemlea?

**Shughuli ya Kikundi Kidogo (Dakika 25)**

Maelekezo ya Mwezeshaji: Wagawe washiriki katika vikundi vya watu 5 hadi 7. Mpe mshiriki mmoja wa kikundi jukumu la kuwa kiongozi wa kikundi kidogo. Mwingine afanye jukumu la Mwalimu wa watu wapya. Waliobaki wafanye kama washirika wa kikundi kidogo. Yasome darasani maelekezo yaliyopo hapa chini. Jibu maswali ambayo washiriki wanaweza kuwa nayo juu ya zoezi hili.

Maelekezo:

1. Kwanza tumia mchezo wa "Ninadhani Hujui Hili" kwa ajili ya kikundi kidogo kutoka katika kikundi cha Kuvunja Ukimya kilichopo hapa chini.
2. Kisha kiongozi wa Kikundi kidogo na mwalimu watachagua swali kutoka kwenye orodha ya Maswali ya Mjadala yaliyopo chini. (Unaweza pia kutumia swali hili "Je, wakati wa furaha zaidi katika maisha yako ulikuwa ni upi?")
3. Baada ya kukamilisha Vivunja Ukimya na Mjadala wa Kikundi, ndipo kikundi kidogo kitapaswa kujihusisha na muda wa kuombeana.
4. Kundi litapaswa kutathimini na kujadili mkutano wa kikundi kidogo. Ikiwa darasa ni dogo, basi darasa zima wafanye hivi kama kundi moja.

**Kikundi Kidogo cha Kuvunja Ukimya**

"Vivunja Ukimya" ni njia za vichekesho, zisizo za kuogopesha za kuwafahamu watu vizuri zaidi. Njia hizi hutumika mara nyingi kwenye wakati wa ushirika wa kikundi kidogo ambacho ni kipya. Mambo ya kuzingatia:

- Kivunja Ukimya kiwe cha kufaa kwa ajili ya kikundi. Ikiwa ni cha kitoto sana, watu hawatajisikia vizuri. Ikiwa ni cha kutisha sana, watu wataogopa.
- Hakikisha kiko wazi kwamba kila mmoja anaalikwa na anatiwa moyo kushiriki.
- Baadhi ya vivunja ukimya vinaweza kutumiwa zaidi ya mara moja.
- Uwe makini kwa watu ambao wanaweza wasijisikie amani na mchezo au shughuli.
- Michezo inakuwa mifupi zaidi na isiyo na umuhimu kadiri kikundi kinavyobanwa zaidi na kozi ya mzunguko wa maisha ya kikundi kidogo. Katika mikutano miwili ya kwanza, unaweza kutumia nusu ya muda katika mchezo lakini baada ya miezi michache unaweza kuhitaji dakika 10 au 15 tu.

Maswali -Ya - Kufahamiana
Ulipokuwa na umri kati ya miaka 7 – 12….

1. Uliishi wapi? Ulikuwa na kaka na dada wangapi?
2. Ni aina gani ya usafiri ambao familia yako waliutumia?
3. Mtu uliyejisikia kuwa karibu naye zaidi alikuwa nani?
4. Ni wakati gani ambapo Mungu alikuwa zaidi ya neno/halisi kwako?

**Mimi ni nani?***
Andika majina ya watu maarufu/na /au wahusika wa Biblia juu ya vipande vya karatasi. Yabandike nyuma ya mgongo wa kila mtu. Mtu hawezi kusoma karatasi yake mwenyewe. Anapaswa kuzunguka chumba akiuliza swali moja kwa wakati mmoja kwamba yeye ni nani mpaka pale anapokisia kuwa yeye ni nani.

*Kwa matumizi ya vikundi vile tu ambavyo watu wote wanaielewa Biblia.

**Ninadhani Hujui Hili**
Kila mtu kwenye kikundi aandike kitu fulani juu ya karatasi nyeupe anachodhani hakuna mtu mwingine kwenye kikundi anayefahamu juu yake. Vipande vya karatasi vinakunjwa, vinachanganywa vizuri, na kupewa namba kwa mfululizo wake. Kisha mtu aliyeandaliwa anaanza kuzisoma, akitaja namba kwanza. Kila mshirika wa kikundi anaanza kuikusanya orodha ya watu ambayo anajisikia inaendana vema na idadi ya kila alama. Baada ya kusomwa kitu cha mwisho, mtu mwenye mlingano mzuri anashinda.

**Utangulizi**
Kila mtu kwenye kikundi anaambiwa kwamba ana dakika kadhaa kufikiria swali na kuuliza kwa habari ya watu wengine kwenye kikundi. Baada ya kila mmoja kulifikiria swali, waanze kugeukiana, wakiuliza maswali yao. Andika jina la mtu na jibu lake. Baada ya dakika kumi, rudini kwenye duara, aandike kitu fulani na kila mtu asimulie kile alichokigundua juu ya watu wengine. Utapata swali lililo bora zaidi, majibu ya ubunifu na yenye kuvutia zaidi.

**Kweli Mbili na Uongo**
Kila mmoja anaandika mambo mawili ya kweli juu yao wenyewe na uongo mmoja. Kisha kila mtu anaamua kipande kipi cha karatasi kilienda na mtu yupi, na ni yapi kati ya maelezo yote yalikuwa ya uongo. Unaweza kuiacha sehemu ya kwanza (yaani kila mtu anashikilia kipande chake cha karatasi na na watu wakisie maelezo yapi ni ya uongo). (Si vema ikiwa mtu atachagua uongo unaokaribiana na ukweli).

**Ripoti ya Hali ya Hewa**
Zunguka duara, ukianzia kwa kiongozi, na uelezee jinsi unavyojisikia sasa hivi kama vile ndio taarifa ya hali ya hewa –mawingu kidogo, vipindi vya jua, nk. Wanafunzi wanaweza kuelezea kwa nini walichagua aina hiyo ya hali ya hewa. Kiongozi anakuwa kielelezo kwa jinsi anavyoguswa wakati wa kushirikisha.

**Kutembea kwa Imani**
Ligawe kundi kwa watu wawili wawili. Mfunike usoni mtu mmoja kwa kila watu wawili. Kila mtu ambaye hajafunikwa anamwongoza aliyefunikwa kuzunguka eneo la mahali pa mkutano. Jaribu kutoa uzoefu wa aina mbalimbali — wapandishe ghorofa kadhaa, toka nje na kuingia ndani, wasaidie kuhisi hali tofauti, tembea katika hatua tofauti, tembea juu ya vitu mbalimbali (majani, sakafu, uchafu) lakini usiseme usiseme lolote baada kuanza kutembea. Wasilisha ujumbe wote pasipo kutumia maneno. Baada ya dakika kama tano, badilisha maeneo. Baada ya dakika tano nyingine, kundi likusanyike tena. Shirikisha aina ya hisia ulizokuwa nazo ulipokuwa umefunikwa usoni na ulipogusa vitu, nk. Ulijisikiaje juu ya mtu mwingine? Hali ilikuwaje kwa kutokuwa na utawala juu ya kile kinachotokea? Ulijifunza nini juu yako mwenyewe? Je, hii inahusiana vipi na uhusiano wako na Mungu? Je, na wengine?

**Mchezo wa Sarafu**
Ikiwa kwa kipindi fulani una watu wapya/wageni kwenye mkutano wako, uutunze Mchezo wa Sarafu kichwani kwa ajili ya kuvunja ukimya. Mpe kila mtu sarafu kumi. Kila mtu ataje kitu kimoja kinachomhusu yeye mwenyewe ambacho ni tofauti na mwingine. (Kwa mfano, kikundi cha uthubutu kinaweza kusema, "Tumepanda hadi kileleni.") Msemaji anaweka sarafu katikati. Ikiwa msemaji mwingine na yeye amepanda hadi Kileleni, na yeye pia anaweza kuweka sarafu. Mtu wa kwanza kumaliza sarafu zake zote anashinda.

**Maigizo ya Timu**
Kwa ajili ya shughuli hii, unahitaji timu mbili na vyumba viwili. Ligawe kundi kuwa timu mbili. Timu A inafikiria vitendo fulani au shughuli kwa ajili ya Timu B ili kuigiza (mfano kula kifungua kinywa) pasipo kutumia maneno yoyote. Timu A inamwambia mtu mmoja tu (tutamwita "Laura") kutoka Timu B kwamba shughuli ni ipi, na Laura haruhusiwi kumwambia mtu mwingine yeyote wa kwenye timu yake. Timu B inasubiri kwenye chumba cha kwanza, wakati Laura anamchukua mtu mwingine kutoka katika timu yake (tutamwita "Michael") kwenye chumba cha pili. Katika chumba cha pili, Timu A inaangalia wakati Laura akiigiza shughuli kwa ajili ya Michael (kumbuka, hakuna kuongea!) Kisha Laura anarudi kwenye chumba cha kwanza na kumtuma mtu mwingine tena kutoka Timu B. Ndipo Michael anaigiza shughuli kwa ajili ya mtu anayefuata, na Michael anarudi chumba cha kwanza na kumtuma mtu mwingine tena kutoka kwenye Timu yake. Mchakato huu unarudiwa, hadi mtu wa mwisho kutoka Timu B anapoangalia shughuli. Ndipo mtu huyu wa mwisho anapaswa kukisia shughuli ni ipi. Hatimaye timu zinabadilishana majukumu na Timu B inafikiria shughuli ambayo Timu A wataigiza.

**Majibu na Waandishi**
Andika maswali manne au matano juu ya vipande vya karatasi ambayo hayatawakosesha amani bali yatakayofunua kitu fulani juu ya mtu (kwa mfano: Mali yako uipendayo zaidi ni ipi? Unatamani ungeliweza kufanya nini ambacho huwezi kukifanya sasa? Muda wako mzuri wa likizo/pumziko ni upi?) Watu wayajibu yote, au angalau matatu, lakini uwaelekeze kutokuweka majina yao juu ya karatasi. Kisha kiongozi anakusanya karatasi na

kuyasoma majibu, na kila mtu anajaribu kukisia ni nani aliyetoa majibu hayo.

**Majirani Zangu Wote**

Kila mtu anaanza kwa kukaa kwenye viti vilivyopangwa kwenye mduara, isipokuwa mtu mmoja ambaye anaanza kwa kusimama katikati ya duara. Mtu aliye katikati anahitaji kutafuta "majirani." Ili kufanya hivi, anahitaji kutoa maelezo yaliyo sahihi juu yake mwenyewe, maelezo ambayo inawezekana yatakuwa sahihi /kweli juu ya mtu mwingine pia kwenye kikundi (kwa mfano "Majirani zangu wote wanapiga kinanda" au "Majirani zangu wote wanatummia mkono wa kuume"). Kila mtu ambaye pia atatoa maelezo haya haya atasimama na kutafuta kiti kingine. Hapaswi kurudi kwenye kiti alichokuwa amekaa. Mtu aliye katikati pia anatafuta kiti, hivyo kila wakati kutakuwa na mtu anayebaki katikati bila kiti. Ndipo, atatoa maelezo ya kweli na kutafuta majirani ambao maelezo haya ni ya kweli na kwao pia.

**Mijadala ya Vikundi**

Chini kuna uchaguzi mwingi wa maswali ambayo yanaweza kutumika wakati wa kuvunja ukimya. Zingatia kwamba baadhi ya maswali haya yanafaa kwa ajili ya vikundi vipya, na baadhi ya maswali yanafaa kwa ajili ya vikundi ambavyo washirika tayari wanafahamiana kidogo. Kwa kawaida, swali moja tu litatumika kwa kila mkutano wa kikundi kidogo. Maswali yanaweza kuchaguliwa kwa sababu yatawasaidia watu kufahamiana vizuri zaidi au kwa sababu yanaendana na mada ya Somo la Biblia kwa ajili ya mkutano huo.

1. Je, ni wakati gani uliokuwa wa furaha zaidi katika maisha yako?
2. Je, ni kitu gani kinachokufanya kujutia zaidi katika maisha yako?
3. Ni kitu gani kilichokuwa kigumu zaidi katika vitu ulivyowahi kufanya?
4. Je, ni sifa gani kubwa uliyowahi kuipokea?
5. Rafiki yako wa karibu zaidi hapa duniani ni yupi? Mwelezee.
6. Ni chumba kipi katika nyumba yako unachokipenda zaidi?
7. Jambo moja unalotaka kulitimiliza juma lijalo ni lipi?
8. Ni wapi ulikojisikia kukirimiwa sana na kuwa salama zaidi ukiwa mtoto?
9. Kama ungepata muda wa kufanya kazi mara moja tu, je, ungefika au ungetembelea wapi katika siku zako za usoni au katika historia?
10. Ni lini ilikuwa mara yako ya mwisho kufanya jambo jipya kwa mara ya kwanza?
11. Kama ungepata dawa ya kukuwezesha kuishi mpaka miaka 1,000, je, ungeitumia? Kwa nini?
12. Je, ungependa kujua tarehe kamili ya kifo chako?
13. Ndugu unayepatana naye vizuri ni yupi? Kwa nini?
14. Kumbukumbu yako nzuri ya muda ulioutumia, kama mtoto, ukiwa pamoja na baba yako ni ipi? Na ukiwa na mama?
15. Je, Mungu alimtumia nani kukufikisha kwenye hatua ambayo ulijua kwamba unamhitaji Yesu?
16. Kama ungeweza kubadilisha maeneo kwa kuwatumia wahusika wa Biblia, je, ungemchagua nani? Kwa nini?
17. Ni kitabu gani cha Biblia unachokipenda zaidi? Kwa nini?

18. Kama ungeliweza kwenda popote katika ulimwengu, je, ungelikwenda wapi?
19. Fikiria nyumba yako inaungua, na familia yako yote iko salama, lakini una muda wa kuchukua/ kuokoa kitu kimoja tu na kutoka nacho. Je, ungechukua kitu gani?
20. Je, ni mkanda au onyesho gani la TV unalolipenda zaidi?
21. Ni nani ameyaathiri zaidi maisha yako tangu tulipokutana kwa mara ya mwisho?
22. Ni kitu gani kizuri sana kilichokutokea wiki hii iliyopita?
23. Taja mtu unayevutiwa naye ambaye alipaswa kuvuka vizuizi vikubwa ili kufika mahali alipo sasa.
24. Ni kitu gani unachokithamini zaidi katika uhusiano wa kibinadamu? Katika uhusiano wako na Kristo? Na wazazi wako?
25. Muda unaoupenda zaidi kwa siku ni upi?
26. (Wasio na wenzi) Elezea aina ya mtu unayependa kumwoa au kuolewa naye. (Walio na wenzi) Ni nini kilichokuongoza kumwoa au kuolewa na mwenzi wako?
27. Ni zawadi gani (ukiacha ya wokovu) ambayo kamwe hutaisahau?
28. Ni tukio gani lililokuwa muhimu zaidi katika maisha yako kwa wiki iliyopita?
29. Kama ungelichagua kwenda popote katika ulimwengu kwa siku tatu, je, ungeliwenda wapi na kwa nini?
30. Kama ungeliweza kuchagua kukutana na mtu yeyote aliyewahi kuishi katika nchi yako, je, mtu huyo angekuwa ni nani, na kwa nini ungelipenda kukutanana naye?
31. Kama ungelichagua kuishi mahali popote katika ulimwengu, je, ungeliishi wapi, na kwa nini?
32. Ni zawadi gani (ya kiroho, kihisia, kiakili, nk.) unaamini unaileta kwenye kikundi hiki? (Kwa maneno mengine, unadhani unaleta/unatoa nini ambacho kitachangia kutiwa moyo kwa watu wengine?)
33. Ni uzoefu gani ulioupitia katika maisha yako ambao ulibadilisha mfumo wako wa kuthamini?
34. Baadhi ya malengo yako kwa mwaka ujao ni yapi?
35. Wazazi wako ni akina nani, wanafanya kazi gani, na nini unachokiheshimu zaidi juu yao?
36. Kama ungeliweza kuchagua kazi tena, je, ungelifanya nini?
37. Kama ungelikuwa kiongozi wa nchi yoyote katika ulimwengu, je, ingekuwa nchi gani na kwa nini?
38. Je, ni uzoefu gani uliokutana nao wiki iliyopita ambao ulikuwa mzuri sana na mwingine uliokuwa mbaya zaidi?
39. Kama ungelipata ziara ya wiki mbili kwenda sehemu yoyote duniani, je, sehemu hiyo ingelikuwa wapi na kwa nini?
40. Kama ungeliweza kuzungumza na mtu yeyote aliye hai, angelikuwa nani na kwa nini?
41. Wape kila mtu kipande cha karatasi na uwaombe kuchora picha ya kazi zao ama chochote wanachofanya kila siku. Elezeeni michoro yenu.
42. Kwa nini una furaha kuwepo kwenye kikundi hiki kidoggo jioni ya leo?
43. Mjulishe kila mtu kwamba amepewa dola milioni moja. Mpe nafasi kila mmoja kushirikisha jinsi atakavyoitumia bahati hii mpya aliyoipata.
44. Je, una jina la utani, na kama ndivyo, ni jina hilo ni lipi? Ni majina gani ya utani uliyona yo kwa ajili ya mwenzi wako na watoto ama ndugu?

45. Je, kuna kipindi katika historia ambacho ungelipenda kuishi kipindi hicho? Na kama ndivyo, ni kwa nini?
46. Je, vikundi vidogo vimekuwa msaada kwako kwa namna gani? Shirikisha ni kwa namna gani na kila mmoja amshukuru mwenzake.
47. Waambie kikundi kidogo mambo matatu unayoshukuru kwa habari ya familia yako na njia tatu ambazo kwazo wanakuwa wagumu kwa nyakati fulani.
48. Ni kitu gani kimoja ambacho hasa ungelipenda kuona kikitokea maishani katika familia yako? Kanisa lako? Kikundi chako kidogo? Ulimwengu?
49. Rafiki yako wa karibu zaidi katika hatua hii ya maisha ni nani?
50. Je, umepokea majibu ya maombi hivi karibuni? Shirikisha kisa hicho.
51. Kazi yako ni ipi? Je, ni kitu gani unachokifurahia juu ya kazi hiyo?
52. Je, ni kitu kimekuwa na athari kuu katika maisha yako ya Kikristo na kwa nini?
53. Je, ni kitabu gani ulichokisoma, filamu, ama video uliyoiona ambayo ungeliipendekeza kwa wengine? Kwa nini?
54. Unadhani ni kitu kinachompendeza Mungu kuliko chochote katika maisha yako?
55. Ni kitu gani cha kutia moyo kilichosemwa juu yako juma hili?
56. Ni tendo gani la kutia moyo ambalo umemtendea mtu fulani juma hili?
57. Ni kitu gani kilichokufanya kuhudhuria katika kanisa hili?
58. Ni kitu gani ambacho bado unapenda kukitimiliza katika maisha yako?
59. Unashukuru kwa kitu gani?
60. Ni tukio gani unalokumbuka zaidi katika maisha yako na kwa nini?
61. Shirikisha Andiko la maana zaidi kwako na kwa nini ni la maana.
62. Je, maisha yako yangelikuwa tofaulti kwa namna gani kama ungelijua kwamba Yesu anarudi baada ya wiki moja?
63. Mtu wa kuvutia zaidi uliyekutana naye ni nani?
64. Muda wa likizo unaokuvutia zaidi ni upi na kwa nini unaufurahia?
65. Shirikisha juu ya uzoefu wako wa kiroho ambao umekuwa nao.
66. Je, unapumzikaje?
67. Ni aina gani ya muziki/wimbo, nk, unaovutiwa nao?
68. Ni kitu gani kilikutokea juma hili ambacho ungelipenda kuwaeleza wana kikundi wengine?
69. Ikiwa usingeliweza kushindwa kitu, ungelipenda kufanya kitu gani?
70. Ikiwa ungelipaswa kuyarudia maisha yako uliyoishi, ungelibadilisha kitu gani?
71. Unatamani nini kiandikwe kwenye jiwe lako la kumbukumbu kaburini?
72. Unatamani nini kisemwe kwenye mazishi yako?
73. Ikiwa ungelipaswa kwenda kuishi mwezini na ukawa na uwezo wa kubeba kitu kimoja tu, ungelibeba kitu gani?
74. Ungelifanya nini ikiwa ungeliona (1) mtu anayeibiwa (2) mtu anayezama na (3) nyumba inayoungua moto?
75. Ni kitu gani kimoja ambacho hukielewi juu ya wanaume (ikiwa wewe ni mwanamke) ama juu ya wanawake (ikiwa wewe ni mwanaume)?
76. Ikiwa ungelipaswa kurudia kitu tena juma hili, ni kitu gani ungelikifanya tofauti?
77. Kielezee kikundi kingine kidogo ambacho ulikuwa mwanachama nje ya Kanisa lako. Kwa nini unafikiri kikundi kilifanikiwa ( ama hakikufanikiwa)? Haujafungwa na vikundi vya “kidini” tu. Wengi wetu tunakutana katika vikundi vidogo kazini.

78. Ni Biblia ipi unayoikumbuka zaidi kati ya ulizowahi kuzipokea (mfano, kwenye ubatizo wako, harusi, ulipookoka, n.k)? Tueleze kwa nini ni ya maana kwako.
79. Ni kitu gani cha kwanza kinachokuja akilini unapofikiria juu ya Mungu?
80. Ni maswali gani makubwa uliyo nayo juu ya uhusiano wako na Mungu?

**Mfano wa Shughuli kwa ajili ya Mikutano ya Vikundi Vidogo**

Ifuatayo ni mifano ya shughuli kwa kila moja ya sehemu nne za mkutano wa vikundi vidogo. Nyakati zilizoorodheshwa kwa kila kazi ni za makisio:

| **Ushirika** | **Kuabudu** | **Kujengana** | **Uinjilisti** |
|---|---|---|---|
| Mtu kwa Mtu | Mtu kwa Mungu | Mungu kwa Mtu | Mwili wa Kristo kwa ulimwengu |
| "Kuelekea Ndani" | "Kuelekea Juu" | "Kuelekea Chini" | "Kuelekea Nje" |
| Dakika 20 | Dakika 20 | Dakika 30 | Dakika 20 |
| • Furahieni shughuli za vichekesho pamoja.<br>• Kuleni chakula pamoja.<br>• Fahamianeni vizuri zaidi.<br>• Tianeni moyo.<br>• Shirikishaneni mambo ya furaha.<br>• Shirikishaneni matatizo.<br>• Ombeaneni ninyi kwa ninyi. | • Imba nyimbo za sifa.<br>• Mshukuru Mungu kwa Ukuu wake.<br>• Mshukuru Mungu kwa yote aliyotenda.<br>• Omba kwa sauti ama kimya kimya.<br>• Soma vifungu vya kuabudu (kwa mfano, Zaburi).<br>• Soma Ushairi wa Kikristo. | • Jifunzeni vifungu vya Maandiko kama kikundi.<br>• Utendeeni kazi ukweli wa Biblia katika hali za kila siku.<br>• Jihusisheni na huduma pamoja na kikundi.<br>• Zigundueni na kuzitumia karama za kiroho.<br>• Karirini mistari ya Biblia. | • Undeni “kikundi cha maombi cha watatu watatu” na mwombe kwa ajili ya wasioamini.<br>• Waalikeni wasioamini kwenye kikundi.<br>• Kama kikundi, kutaneni na mahitaji ya watu wanaowazunguka.<br>• Kuzeni ushirika na watu wasioamini.<br>• Washirikisheni wengine Habari Njema. |

**Chakula cha Mchana (Dak. 60.)**

# KIPINDI CHA 4
# KULICHAMBUA NENO LA MUNGU KWA KUTUMIA MAFUNZO YA BIBLIA KWA NJIA YA UCHIMBUZI

A. ________________– Je, inasemaje?
B. ________________ – Je, ina maana gani?
C. ________________ – Je, ninapaswa kufanya nini?

**Uchunguzi – Andiko Linasema Nini?**

a. ________________ Kuchunguza Kwa Uangalifu Kile Ambacho Andiko Linasema

- Ni nini jukumu la Roho Mtakatifu? 1 Kor. 2:14
- Ni nini jukumu ama kazi ya maombi? Waefeso 1:18
- Ni nini jukumu la utayari wa kutii? Yakobo 1:22-25
- N nini jukumu la kujipima katika nuru ya kifungu kilichofundishwa? 2 Kor. 13:5
- Ni nini jukumu la utayari katika kujifunza? Matendo 17:11

b. Pata _____________wa Kutosha.

- Muda wa kutosha ni muda gani?
- Ni wakati gani ulio mzuri kwako usioingiliwa ama kukatishwa kwa ajili ya kujifunza Neno la Mungu?
- Ni mahali gani palipo bora kwa ajili yako ili kuwa na muda wa kujifunza Neno la Mungu pasipo kuingiliwa ama kukatishwa?

c. Angalia ________________________________(ama hali)ya Andiko
Pima yafuatayo:

- Mistari iliyotangulia na inayofuata inazungumzia nini?
- Somo la kifungu ni lipi?
- Kiini/Somo kuu la sura ni lipi?
- Kusudi na somo la kitabu ni lipi?

d. Pima _____________ wa Andiko

- Andiko lina uandishi gani?
- Maneno ya msingi ni yapi?
- Ni mambo yapi yana mlingano na yapi yana utofauti? Ni kwa jinsi gani mawazo yanakua unapolisoma andiko?
- Kuna vitenzi gani? (Vinazungumzia kitendo ni kipi.)
- Kuna viunganishi gani na viko wapi? (Vinaonyesha mpito kutoka mada moja kwenda nyingine.)
- Kuna mafafanuzi gani?

e. Uliza Maswali ya ________________ ya Andiko
Uliza maswali juu ya andiko ambayo mwana habari angelimwuliza shahidi aliyeshuhudia tukio:

- Nani?
- Nini?
- Wapi?
- Lini?
- Vipi?
- Kwa nini?

**Onyesho/Mfano wa Kujifunza Biblia kwa Njia ya Uchimbuzi – Uchunguzi**
Maswali ya Kiutafiti:

**Nani?**
- Mwandishi wa sehemu hii ya Andiko ni nani (mstari wa 1)?
- Ni watu gani waliotajwa katika kifungu hiki (mstari wa 5)?
- Ni nani anayeongea katika mstari wa 5?
- Ni watu gani waliotajwa katika muktadha wa kifungu hiki (mstari wa 1-3)?
- Maswali mengine yanayoanza na "Nani...?"

**Nini?**
- Matukio ya msingi katika muktadha wa kifungu hiki ni yapi?
- "Neno la Bwana" lililomjia Yeremia lilikuwa ni lipi (mstari wa 5)?
- Ni matendo gani mahsusi manne ambayo Mungu anasema aliyafanya katika mstari wa 5?
- Katika mstari wa 5, jukumu la Yeremia lilipaswa kuwa ni nini?
- Jukumu la Yeremia lilikuwa na upana gani kulingana na mstari wa 5? Lilikuwa ni kwa taifa la Israeli tu au lilikuwa pana zaidi?
- Mwitikio wa Yeremia katika mstari wa 6 ulikuwa ni upi?
- Mwitikio au jibu la Mungu kwa Yeremia lilikuwa ni lipi kulingana na mstari wa 7-8?
- Ni maelekezo gani mawili ambayo Mungu anampa Yeremia kulingana na mstari wa 7-8?
- Yeremia alikuwa na chaguzi gani kulingana na mstari wa 7?
- Hisia ya Yeremia ambayo Mungu anaizungumzia katika sehemu ya kwanza ya mstari wa 8 ni ipi?
- Sababu mbili za kutokuogopa zinazotolewa kwa Yeremia ni zipi (mstari wa 8)?
- Bwana anafanya nini kwa Yeremia katika mstari wa 9?
- Mstari wa 10 unaelezea kazi ya Yeremia. Misingi ya kazi yake ilikuwa ni nini?
- Ni mfululizo gani wa matukio uliotajwa katika mstari wa 10?
- Mungu anafanya nini katika mistari inayofuata andiko hili(mistari 11-16, 17-19)
- Maswali mengine ya "Nini...?"

**Wapi?**
- Muktadha unarejea wapi (mstari 1)?
- Sehemu hizi ziko wapi?

- Inaelekea Yeremia alikuwa wapi wakati akipokea wito huu kutoka kwa Bwana (mstari wa 1)?
- Maswali mengine ya "Wapi...?"

**Lini?**
- Ni kipindi gani cha wakati kilichoelezwa katika maudhui yote ya kitabu hiki?
- Katika mstari wa 5, Mungu alijua (alimchagua) lini Yeremia?
- Katika mstari wa 5, ni lini Mungu alimtenga Yeremia kwa ajili ya huduma?
- Maswali mengine ya "Lini...?"

**Kwa nini?**
- Kwa nini Mungu anamwita Yeremia?
- Kwa nini kazi ya Yeremia kama nabii ni ya muhimu?

**Vipi?**
- Yeremia ameelezewa vipi katika mstari wa 1?
- Baba yake Hilkia ameelezewa vipi katika mstari wa 1?
- Yeremia anamwelezea vipi Mungu katika mstari wa 6?
- Yeremia anaitikia vipi neno la Mungu katika mstari 6?
- Mungu anamwelezea vipi Yeremia katika mstari wa 18?

**Maandalizi ya Somo la 3:**
**Kujifunza Biblia kwa Njia ya Uchimbuzi – Uchunguzi**
Ikiwa haukupata muda wa kumaliza uchunguzi wa Yeremia 1:4-10, fanya hivyo kabla ya somo linalofuata. Angalia ikiwa unaweza kuuliza maswali mengine yanayofaa kwa kifungu kile kile. Yatunze maswali na majibu haya kwa matumizi ya kipindi kinachofuata.

# KIPINDI CHA 5
# JINSI YA KUHAMASISHA MAOMBI KWA AJILI YA KANISA LAKO LILILOPANDWA.

**Maombi:**
**Kipengele Muhimu cha Uinjilisti na Upandaji wa Kanisa**

Kwa kutumia maandiko yafuatayo, gundua na kujadili sababu za Kibiblia zinazoonyesha kwamba maombi ni ya muhimu katika uinjilisti na upandaji wa Kanisa.

Warumi 10:1
Waefeso 6:18
Waefeso 6:19-20
Wakolosai 4:2-4
2 Wathesalonike 3:1-3

Jinsi ya Kuyahusianisha Maombi pamoja na Uinjilisti na Upandaji wa Kanisa.

1. Katika ________________________
2. ____________________________ – waumini watatu kuomba pamoja.
3. ___________________________ – kuzunguka eneo unalopanga kutoa huduma, ukitulia na kuomba kimya kimya katika maeneo fulani.

**Mjadala wa Maombi ya Kutembea (Dakika 15)**

**Kisa na Mkasa 1:**

Jamii jirani iliyojulikana kuwa na lundo kubwa la familia zenye matatizo lililengwa kwa ajili ya kufungua Kanisa. Matatizo ya kijamii kama kukosa ajira, kuvunjika kwa familia, madawa ya kulevya, na uhalifu ulikuwa ni kawaida sana. Katika sehemu ya kwanza ya jitihada ya upandaji wa Kanisa, maombi ya kutembea yalipangwa kwa kila mtaa katika jamii. Wakristo walipokuwa wakitembea na kuomba, walinukuu kila nuru/mafunuo ambayo Roho Mtakatifu aliwapa. Maombi mengine ya kutembea yalifuata baada ya yale ya kwanza. Baadhi ya maombi ya kutembea yalifanyika kuzunguka shule, mengine ndani ya soko na kuzunguka eneo la soko, na mengine katika ukingo wa nje wa jamii/ujirani. Maombi mengine ya kutembea yalifanyika katika eneo la misitu inayotazamana na jamii. Kwenye misitu hii, mahali palipojulikana kutolewa madawa ya kulevya, alama za uchawi zilionekana juu ya miti. Timu ya maombi ya kutembea ilitumia muda kuomba kinyume na nguvu hizi za uovu. Kwa miaka mitatu tangu jamii hii ilipolengwa kwa ajili ya upandaji Kanisa, matatizo ya kijamii yameondoka, uhalifu umepungua kwa 40%, na Kanisa la watu 70-80 limepandwa. Sasa kuna ushawishi mzuri wa kiroho unaosambaratisha uovu, na Mungu anatenda kazi katika maisha ya watu walio wengi. (DAWN Europa Prayer Manual, August 1994, pg. 13).

- Ni mawazo gani ungependa kushirikisha kama mwitikio wa kisa na mkasa huu?
- Ni faida gani zilizo kubwa zaidi kutokana na aina hii ya maombi ya kutembea?
- Changamoto kubwa zaidi zingekuwa ni zipi?

**Kisa na Mkasa 2:**
Mpanda Kanisa na familia yake walihamia kwenye nyumba ya ghorofa ndani ya jiji mahali walipotamani kuona kanisa limeanzishwa. Muda wa jioni sana, familia ilitembea pamoja kwenye jengo la ghorofa. Walisimama mbele ya mlango wa kila ghorofa na kila mwana familia aliomba kwa ajili ya watu wanaoishi kwenye ghorofa hiyo. Kijana mdogo aliomba kwamba kila mtu kwenye nyumba ya ghorofa amkaribishe Yesu moyoni mwake. Binti mmoja aliomba Mungu akutane na mahitaji ya kifedha ya familia, binti mwingine akaomba kwa ajili ya mahusiano mazuri ya kifamilia. Mama aliomba kwa ajili ya afya kwa wana familia na baba akaomba baraka za Mungu zishuke juu ya nyumba hiyo. Baada ya maombi ya kutembea, mpanda Kanisa na familia yake waliona watu 14 katika nyumba hiyo ya ghorofa wakimjia Kristo na Kanisa dogo likaanza.

- Ni mawazo gani ungependa kushirikisha kama mwitikio wa kisa na mkasa huu?
- Ni faida gani zilizo kubwa zaidi kutokana na aina hii ya maombi ya kutembea?
- Changamoto kubwa zaidi zingekuwa ni zipi?

**Timu ya Msaada wa Maombi**
- Je, una timu ya watu wanaoomba kwa ajili ya huduma yako ya upandaji wa Kanisa? Je, inakusaidiaje? Je, unahitaji timu yako wakuombee juu ya nini?
- Ni kwa njia zipi utaendelea kuijulisha timu yako ya msaada wa maombi juu ya mahitaji ya kuombea na majibu ya maombi?
- Ni aina gani ya taarifa unadhani zingekuwa bora kuwashirikisha timu ya waombaji na ni aina gani ya taarifa zisingepaswa kushirikishwa?
- Ni maoni gani mengine ya kukusaidia kuongeza maombi kwa ajili ya huduma yako ya upandaji wa Kanisa?

**Kukusanya Taarifa kwa Ajili ya Maombi**
- Ni aina gani ya taarifa ambazo zingeweza kukusanywa katika utafiti zingeliweza kufaa sana kwa ajili ya maombi ya mtu mmoja mmoja au jamii?
- Je, taarifa kama za makanisa yaliyopo katika eneo, occultist ama makundi ya imani za kishetani yaliyopo, ukuaji wa kanisa, na umoja wa waumini zinaweza kufaa kwa maombi yako. Eleza kwa nini?

**Maandalizi ya Funzo/Somo la 3:**
**Timu ya Msaada wa Maombi na Ujuzi wa Maombi ya Kutembea**

1. Anzisha timu ya msaada wa maombi ikiwa bado hujafanya hivyo. Waombe angalau watu watatu ili waiombee huduma yako kila wiki. Je, utaendelea kuwajulisha kwa namna gani juu ya mahitaji yako ya kuombea na majibu ya maombi?
2. Fanya angalau maombi ya mara moja ya kutembea katika eneo lako lengwa pamoja na timu yako ya upandaji wa Kanisa au wengine wenye mzigo wa kuona eneo hilo

limefikiwa kwa ajili ya Kristo. Jadili ujuzi huu na mlezi au mkufunzi wako.

| **MALENGO YA UPANDAJI KANISA KWA MWEZI HUU** | |
|---|---|
| **MTU MMOJA MMOJA** | |
| Watu wapya waliofikiwa | Tafadhali Weka Idadi |
| Watu wapya Waliokata shauri | Tafadhali Weka Idadi |
| Watu wapya Waliobatizwa | Tafadhali Weka Idadi |
| Viongozi Wapya Wanaofunzwa | Tafadhali Weka Idadi |
| **VIKUNDI VIDOGO** | |
| Vikundi vidogo vipya | Tafadhali Weka Idadi |
| Washiriki wapya kwenye vikundi vidogo | Tafadhali Weka Idadi |
| Viongozi wapya kwenye vikundi vidogo | Tafadhali Weka Idadi |

- Omba watu wa kujitolea ili washirikishe majibu ya maswali yafuatayo kwa maneno yao wenyewe:
  1. Sababu tatu za kitheolojia za kupanda makanisa ni zipi?
  2. Je, Kutengeneza Ramani ya Kiroho ni nini na kwa nini ni muhimu?
  3. Alama nne za mikutano ya vikundi vidogo ni zipi na mipangilio yake ni ipi?
  4. Tunapojihusisha katika uchunguzi wa sehemu ya somo la uchimbuzi wa Biblia, je, tunachunguza nini?
  5. Baadhi ya njia za kiutendaji ambazo kwazo unaweza kuhamasisha maombi kwa ajili ya jitihada yako ya upandaji wa Kanisa ni zipi?

**Pumziko (Dk. 15.)**

# KIPINDI CHA 6
# TAMASHA LA MAOMBI

**Tamasha la Maombi ni nini?**

Neno "Tamasha la Maombi" linatoka mwanzoni mwa miaka ya 1700 na limekuwa likitumika katika vizazi vilivyofuata kuelezea harakati kubwa za maombi zinazoendelea katika kizazi kipya kwa ajili ya kuuendeleza ufalme wa Mungu. Katika kitabu cha *The Eager Feet,* Dr. J. Edwin Orr anaandika: "Tamasha la Maombi kwa ajili ya uamsho katika miaka ya 1780 huko Uingereza na miaka ya 1790 huko Marekani, na Matamasha ya Kufanywa Upya katika nchi zote mbili…yalidhihirisha kwa uwazi kuwa ndio sababu kuu ya kuwahamasisha na kuwaandaa Wakristo kwa ajili ya huduma katika harakati za ulimwengu wote ambazo zilififisha kabisa nguvu za kijeshi katika vita ya Waterloo. Kama ilivyo katika nusu ya kwanza ya karne (mwanzoni mwa miaka ya 1800), maono ya kila mmishonari kiutendaji (kuanzia mwaka 1858 na kuendelea) yaliasisiwa na watu waliohuishwa katika uamsho wa makanisa yanayowatuma."

Tukizungumza kihistoria, lengo la msingi la Matamasha limekuwa likilenga ajenda kuu mbili: 1) Wakristo waliomba kwa ajili ya Ukamilifu wa Kristo kudhihirishwa ndani ya Kanisa Lake ili kuwatia nguvu kutimiliza kazi iliyokuwa mbele yao. 2) Vilevile waliomba kwa ajili ya utimilifu wa makusudi yake ya kuokoa kati ya mataifa kwa njia ya kanisa lenye uamsho na lililojitoa. Ajenda hizi hizi mbili ndizo zinazotakiwa kukaziwa hata leo.

Na kwa hiyo, "Matamasha ya Maombi" husaidia kuwatambulisha Wakristo waliounganana pamoja kwa mtindo endelevu ili kuutafuta ukamilifu na utimilifu. Maombi yasiyo ya kawaida, ya watu waliounganana, hayatambuliwi kwa namna mtu anavyoomba muda mrefu au anavyoomba mara nyingi kiasi gani, bali hasa ya kwamba Wakristo wanaomba, na wanapoomba, wanaombea yale mambo yanayougusa zaidi moyo wa Mungu, na kwamba wanafanya hivyo kwa pamoja - "katika tamasha."[1]

Leo "Tamasha letu la Maombi" linasimamia Zaburi ya 95. Zaburi hii inatuongoza kupitia hatua tatu, kama ilivyoonyeshwa katika mchoro uliopo hapa chini:

| **Zaburi 95** | |
|---|---|
| 1. Mwimbie Bwana | mst. 1-5 |
| 2. Piga magoti mbele za Bwana | mst. 6-7 |
| 3. Msikilize Bwana | mst. 8-11 |

[1] *The Traveling Team* (2012). "What is a 'Concert of Prayer?'" retrieved from http://www.thetravelingteam.org/ articles/concert-prayer.

# NJOONI TUPIGE MAGOTI, TUMWABUDU
# TAMASHA LA MAOMBI
# LIMESIMAMIA ZABURI YA 95

## I. Mfanyieni Bwana Shangwe: Soma Zaburi ya 95:1-5

Njooni Tumwimbie Bwana kwa Furaha

- **Imbeni** nyimbo za furaha.
- **Mshangilieni** Mwamba wa Wokovu wetu.
- **Someni Pamoja** kwa sauti kutoka katika Zaburi ya ukombozi: Zaburi 18:1-3, 30-36.
- **Njooni** mbele za Bwana kwa kushukuru.
- **Muwe na muda wa ushuhuda**, hasa kumshukuru Mungu kwa yale anayotenda katika maombi ya utatu na maeneno mengine ya upandaji wa Kanisa.
- **Mtukuzeni** Bwana kwa Muziki na Kuimba: Muwe na muda mwingine wa kumwimbia Bwana nyimbo za sifa.
- **Someni pamoja** mstari wa 3-5 wa Zaburi ya 95; **Mshukuru** kwa utawala Wake Mkuu juu ya dunia yote.

## II. Mwabuduni Bwana: Soma Zaburi 95: 6-7

- **Pigeni Magoti**...Piga magoti mbele za Bwana Muumbaji wetu (jaribu kuruhusu viungo vya mwili kuakisi andiko na hali ya Zaburi inayobadilika).
- **Watie moyo** wanafunzi kuomba kwa roho ya unyenyekevu. Wakijisikia kupiga magoti, waruhusu kufanya hivyo.
- **Yeye Ndiye Mungu Wetu**...Sisi ni Watu wa Malisho Yake.
- **Mshukuru** kama Mchungaji Wako. Mtukuze kwa kukutunza.
- **Mwombe** alainishe moyo wako ili uweze kumsikia anaponena.

## III. Sikiliza Sauti Yake, Usifanye Moyo Wako Kuwa Mgumu. : Soma Zaburi ya 95: 8-11

- Ungama dhambi yoyote iliyo dhahiri katika maisha yako. Soma 1 Yohana 1:9.
- Pata muda wa kumsikiliza Bwana. Mwombe akuonyeshe ikiwa kuna maeneo ambayo unahitaji kuondokana na mifumo ya kale, tabia, au mitindo ya upandaji wa kanisa inayoonekana haifai kulingana na muktadha wako kama matokeo ya Andiko ulilolijifunza katika somo hili. Mng'anganie Mungu kwa maeneo yale anayopenda uyaendeleze na yale anayopenda ubadilike katika maisha na katika huduma yako.
- Soma Waebrania 3:7-19. Mstari wa 13 unatuambia tutiane moyo sisi kwa sisi kila siku. Jigaweni katika vikundi vya watu wawili au watatu. Ombeaneni maombi ya kutiana moyo kila mmoja kwa mwenzake.
- Fungeni kwa wimbo na maombi ya baraka kwa wapanda kanisa.

# KUFUNGA

Waombe washiriki kusimulia kitu walichojifunza kwenye mafunzo ambacho kiliwasisimua, kiliwatia moyo au kuwapa motisha kwa ajili ya kazi yao kama wapanda kanisa.

**Nini kinachofuata?**
**Ni nini kinachofuata?**

Kabla hujafika kwenye kipindi cha mafunzo kinachofuata, tunapendekeza ufanye yafuatayo:

- Kutana/Fikia watu 10 wapya.
- Peleka injili kwa watu 5.
- Anzisha kikundi kidogo kipya.

Mpango Kazi kwa ajili ya Somo #3: Mambo Muhimu:

- Kamilisha Shughuli ya Kutengeneza Ramani ya Kiroho (angalia Kipindi cha1).
- Andaa na kuwashirikisha ushuhuda wako watu 5 wasioamini (angalia Kipindi cha 2).
- Ikiwa hukupata muda wa kukamilisha mafunzo ya Biblia kwa njia ya uchimbuzi katika Yeremia 1:4-10, fanya hivyo kwenye kipindi cha mafunzo kinachofuata (angalia Kipindi cha 4).
- Ipange Timu yako ya Msaada wa Maombi na mwende kwenye maombi ya kutembea (angalia Kipindi 5).